Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Itikadi na Uwezo wa Kijinsia katika Nyimbo za Taarab

Mary M. Malenya[1]; Sheila Pamela Wandera Simwa[2]; James O. Ogola[3]

[1]Chuo Kikuu Kishiriki cha Marafiki cha Kaimosi
Idara ya Lugha na Fasihi, Kenya
[2,3]Idara ya Fasihi, Lugha na Mawasiliano
Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya
[2]sheiwande@gmail.com; [3]a9904279@yahoo.com

Main Author Email: marymalenya5@gmail.com

IKISIRI

Makala haya yalilenga kuchunguza itikadi inavyomsawiri mwanamke huku ikimpokonya uwezo wa kutekeleza majukumu sawa na mwanamume. Itikadi ndio huwaongoza watu namna wanavyotumia lugha na hivyo kudhihirisha mahusiano ya mamlaka. Usemi huu unadhibitisha hoja zinazowaongoza watunzi wa fasihi hivi kwamba lugha wanayotumia ndio hubainisha nafasi anayopewa mwanajamii. Suala hili liliwezeshwa kwa kuwepo na malengo mawili. Moja, kuchunguza utunzi na maudhui tawala katika nyimbo teule za taarab ili kubaini mafungamano ya masuala hayo na itikadi inayotawala. Pili, kuonyesha mahusiano ya uwezo kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii kupitia nyimbo za taarab. Malengo haya yaliafikiwa kupitia uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika nyimbo mbili teule za taarab ili kuonyesha usawiri wa mwanamke kwa kuzingatia itikadi na uwezo wa kijinsia. Nyimbo zilizochanganuliwa ni *Daktari wa Mapenzi* na *VIP* ambazo zimeimbwa na Mzee Yusuf akiwa na *bendi ya Jahazi Modern Taarab* nchini Tanzania.Vigezo vikuu vya uteuzi wa nyimbo hizi ni maudhui na lugha. Nadharia zilizotumika ni ufeministi wa Kiafrika inayorejelea masuala ya jinsia ya kike pamoja na Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) itakayochunguza matumizi ya lugha. Data za makala haya zilikusanywa kwa kuchanganua nyimbo teule. Mtafiti alisikiza kanda ili kupata matini za kumfaa katika ukusanyaji data. Data iliyokusanywa ilifanyiwa unukuzi, kuainishwa, kupangwa, kuchanganuliwa na kufasiriwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia mbili zilizotumika katika utafiti huu. Data hiyo iliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Maneno muhimu: *Itikadi, jinsia, uwezo, nyimbo*

How to cite this article in APA (6th Edition)

Malenya, M.M., Simwa-Wandera, S.P., &. Ogola, J.O. (2020).Itikadi na Uwezo wa Kijinsia katika Nyimbo za Taarab. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 48-60.

---***---

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Utangulizi

Fairclough (1995) anadhibitisha kwamba lugha wanayotumia watunzi wa kazi za fasihi ndio hubainisha nafasi anayopewa mwanajamii na majukumu anayopaswa kutekeleza. Utafiti huu umechangia kazi yetu kwa sababu tumetumia kipengele cha lugha na jinsia kuangalia itikadi inavyohusishwa katika kumsawiri mwanamke na matokeo yake. Kwa mujibu wa Wodak na Meyer (2001), mtazamo wa kihistoria unaweza kujaribu kueleza diskosi na jamii, mamlaka na itikadi. Mamlaka na itikadi ni mambo yanayotangulia kuwepo kwa matini na hivyo ni vyema kuchunguza historia ya utamaduni wa jamii fulani ili kuona itikadi fulani na mahusiano ya mamlaka yalivyokuwa na yanavyoendelezwa hadi leo. Utafiti huu umetufaa katika kufafanua namna itikadi na mamlaka inavyotumika kumsawiri mwanamke. Watunzi wa taarab wanazingatia matumizi ya tamathali za semi ambapo baadhi ya semi hizo huchukua maana zinazohitaji uchanganuzi wa kina ndipo zipate kueleweka na kutoa ufafanuzi wa sura ya mwanamke katika jamii (Yego, 2011).

Mapitio ya Maandishi

Momanyi (2001) anadokeza kuwa katika jamii ya Waswahili kuna itikadi zinazohalalisha mamlaka ya mwanamume kwa misingi ya desturi za kitamaduni, itikadi za kidini na tofauti za kijinsia. Katika muktadha huu mwanamume ana nafasi zifuatazo katika jamii: Kwanza, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria. Pili, wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini. Tatu, desturi za jinsia ya kiume zimehalalishwa kwa madai kuwa wanaume husukumwa kutenda kulingana na ubabedume. Aidha, nguvu za mwanamume zinajidhihirisha kama nguvu za kimwili, shujaa, kufanya kazi na kukidhi familia, kuwa na tajriba, mkakamavu, razini, anayejitakia makuu, majivuno, mwadilifu na mshindani. Kwa upande mwingine, jamii za Kiafrika humtukuza mwanamume kupitia mila, desturi na itikadi zao (Kobia, na Mung'ahu, 2011).

Nyimbo za taarab zilitumika kama chombo cha kupinga masuala ya kijamii kama vile utabaka uliokuwa ukiendelezwa na utawala wa Kiarabu pamoja na uwekwaji pembeni wa wanawake. Siti Binti Saad mwanamke wa kitumwa alikuwa wa kwanza Zanzibar kuziimba na hivyo kuvunja kaida kuwa zilikuwa nyimbo za kutungwa na kuimbwa na wanaume tu kwa kuwatenga wanawake, itikadi ya ubabedume ilikuwa ikijitokeza bayana (Igobwa, 2007). Anapozungumzia masuala ya kijamii katika utafiti wake, Igobwa (2007) anatupatia ilhamu ya kutaka kufanya utafiti wa kina katika kupambanua masuala ya kijinsia yanayomuathiri mwanamke.

Kinge'i (1992) amechunguza nafasi ya taarab katika lugha, utamaduni na mawasiliano katika jamii kati ya 1963-1990. Amechanganua maudhui katika nyimbo za taarab ikiwemo siasa, taswira ya mwanamke na mazingira mbali mbali ambamo uimbaji wa nyimbo za taarab umejikita. Utafiti wake umetoa mchango mkubwa katika utafiti huu ambao umetumia taswira ya mwanamke kuibua masuala ya udunishaji wa mwanamke. Tumechunguza lugha inavyotumika katika taarab tukiegemea zaidi kwenye suala la itikadi na uwezo wa kijinsia kwa mtazamo wa kifeministi. Ntarangwi (1998) ameshughulikia nyimbo za taarab, uana na dini kwa msingi wa utamaduni wa Waswahili. Amechunguza namna muziki wa taarab hutumika katika kubeba vipengele vya kitamaduni vya dini na uana. Pia ameshughulikia historia ya taarab, muktadha wa utendaji

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wake pamoja na kuendeleza masuala ya kijinsia katika muziki wa taarab. Utafiti wake umetufaa pakubwa pale anaporejelea historia ya taarab pamoja na masuala ya kijinsia kwa kutupatia matini rejelezi.

Misingi ya Nadharia

Nadharia ya ufeministi ni nyenzo muhimu katika uchunguzi wa masuala ya jinsia kama yanavyojitokeza katika kazi za Fasihi. Ni nadharia yenye mchango mkubwa katika kufanikisha harakati za ukombozi wa mwanamke. Ni jina linalomaanisha ukombozi wa mwanamke huku likijumuisha aina nyingi za misimamo mbali mbali pamoja na matapo na itikadi zinazonuia kutetea haki za wanawake. Nadharia ya ufeministi ni tukio la mavuguvugu ya kifeministi ambayo inahusu nadharia za asili ya ukosefu wa usawa, na wakati mwingine, picha iliyojengwa na jamii kuhusu jinsia na uana, katika taaluma tofauti. Wanaharakati wa ufeministi wanapigia debe haki za wanawake kama vile mikataba, mali, na upigaji kura. Wanapinga vita katika familia, dhuluma za kimapenzi na ubakaji. Katika uchumi, wanatetea haki kazini, ujira sawa na nafasi za kazi na kuanzisha biashara (Wafula, na Njogu, 2007).

Showalter (1977) anasema ufeministi asilia ulianza kushughulikiwa tangu karne ya kumi na nane na umepitia mikondo tofauti. Mkondo wa kwanza (karne ya 19 na 20) ulilenga kupiga vita maonevu dhidi ya mwanamke kwa kutetea haki yake. Mkondo wa pili ulioibuka kati ya (1960-1980) ulinuia kupinga ubaguzi wa mwanamke kijamii na kitamaduni kuondoa sheria za kijinsia zilizowakandamiza na kutetea jukumu la wanawake katika jamii. Mkondo wa tatu ulizuka kati ya (1990-2000) ili kushughulikia aina mbali mbali za ufeministi zilizoibuka. Showalter (1977) alidai kuwa uhakiki wa kifeministi hutofautiana na misimamo ya sasa ya nadharia za uhakiki kwa kuwa haupati misingi yake ya kifasihi kutokana na mamlaka moja au katika matini takatifu. Uhakiki wa kifeministi unaaminiwa kuwa ulitokana na viini kadha kupitia usomi wa fasihi zinazohusu wanawake, kupitia mabadilishano baina ya wana-nadharia wa ufeministi katika masomo mengine, mathalan historia, anthropolojia, saikolojia na kutoka udurusu na urejelezi wa nadharia ya fasihi yenyewe. Mivutano ya rangi ya Kiafrika na utamaduni inajitosheleza katika ufeministi wa Kiafrika katika mkondo wa tatu wa ufeministi.

Wafula na Njogu (2007) wanadai kuwa masuala ya kifeministi yalianza kuzungumziwa katika karne ya 19 na kuanza kutia fora katika miaka ya 60 na 70 ambapo wanawake wa magharibi walianza kuzungumzia matatizo yao katika machapisho. Miongoni mwa kazi zinazorejelewa katika kulimulika suala la ufeministi ni *A Room of One's Own* (Woolf, 1929) na *A Vindication Of The Rights Of Women* (Wollestonecraft, 1792).

Wollstonecraft alidai kwamba matatizo ya mwanamke yanatokana na mielekeo hasi kumhusu mwanamke ambayo inatokana na elimu duni anayopewa na mwanamume. Chapisho jingine la *The Second Sex* (1952) lililochapishwa na Simone de Beauvoir lilichangia zaidi katika maendeleo ya uhakiki wa kifeministi. Beauvoir alibainisha, kukosoa na kuzipiga vita asasi za dini, ndoa na utamaduni zinazomdhalilisha mwanamke. Naye Germaine Greer katika kitabu chake *The Female Eunuch* (1971) akawahimiza wanawake kususia ndoa kwa sababu hali ya kuolewa inawafanya kumilikiwa na kukosa ubinafsi na uhuru wao.

Baadhi ya mihimili ambayo ni ya kimsingi ni: mosi, ufeministi ni tapo linalolenga kuleta usawa katika masuala ya utamaduni na uana ambapo linapigania jamii mpya yenye misingi katika amali za kibinadamu. Amali hizo ni za kike na za kijadi ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa. Mhimili huu ulituwezesha kutambua baadhi ya masuala yanayochangia mwanamke kudharauliwa na

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

hata kunyanyaswa katika jamii kupitia kwa nyimbo za taarab.

Pili, tapo hili hutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kiyakinifu hali anamojikuta mwanamke ili kuwawezesha watu wengine kuielewa hali hiyo. Nyimbo za taarab katika utafiti huu ni mwafaka katika kuchunguza na kuelezea hali ya mwanamke katika jamii. Tuliutumia mhimili huu kuonyesha namna suala la ubabedume linavyopewa nafasi fiche wakati ndilo kero katika maisha ya wanawake na ndicho chanzo cha harakati za wanawake katika kutaka kujikomboa ili waweze kujikwamua maishani.

Tatu, tapo hili linajaribu kuwahamasisha waandishi mbalimbali wa kazi za fasihi kuandika kazi za sanaa ambazo zina wahusika wa kike wa kuigwa ili wawe mfano wa wanawake wanaoweza kujitegemea, kinyume na pale ambapo muda mrefu wanawake wamepewa taswira ya kumtegemea mwanamume. Mhimili huu ulitufaa katika kuweza kutambua kazi mbali mbali zilizoandikwa na wanawake na matokeo ya usomaji wa kazi hizo kwa wanawake.

Nne, tapo hili linajaribu kukuza na kuendeleza hisia za umoja kati ya wanawake ili waweze kupendana na kuondoa dhana ya kuwa wanawake hudhulumiana wenyewe kwa wenyewe. Vile vile ni mtazamo unaonuia kuzindua mwamko kwa upande wa jinsia ya kike wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine (Wafula, na Njogu, 2007). Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza ubora au upungufu uliopo kati ya mahusiano yao na wanaume na endapo matokeo yake ni unyanyasaji, ikiwa ndio msingi wa utafiti wetu.

Tano, tapo hili linajaribu kuonyesha kuwa ikiwa mwanamke anaonekana kudunishwa inafaa mikakati ibuniwe ili aweze kutumia udunishaji huo kupigania haki yake. Mhimili huu ulitusaidia kubaini nafasi ya mwanamke na hivyo kumpa uwezo wa kushindana na mwanamume katika ujenzi wa taifa. Utafiti huu uliongozwa na tawi la ufeministi wa Kiafrika ambalo linapigania haki na ukombozi wa mwanamke pamoja na kumalizika kwa ubaguzi wa kijinsia.

Ufeministi wa Kiafrika

Utafiti huu umejadili itikadi na uwezo inavyojitokeza katika matini za taarab. Kwa kuzingatia msingi wa maeneo ya kijiografia tumejikita katika fasihi ya Kiafrika. Hili ni eneo ambalo lilipuuzwa na waasisi wa nadharia ya ufeministi huku wakiegemea maeneo ya Uingereza, Ufaransa na Marekani. Ingawa ufeministi wa Kiafrika unahusu masuala ya Kiafrika uliendelezwa na mataifa ya Kimagharibi kupitia kwa wanawake wa rangi nyeusi na wenye asili ya Kiafrika. Mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika amesawiriwa kama kiumbe dhaifu na ametengewa nafasi inayoonekana kuwa duni lakini yenye majukumu mengi.

Kwa msingi huu ni wazi kuwa mwanamke anayeithamini ndoa na watoto wake huhiari kudhulumiwa na mumewe kwa vyovyote vile ili kudumisha ndoa yake. Leslie Ogundipe katika (Adeola, 1990) anaeleza kwamba, "Katika jamii ya ubabedume, wanawake kwa kukusudiwa wanabebeshwa majukumu maradufu au zaidi ya yale ya wanaume. Ufeministi wa Kiafrika ni tapo linalojikita katika misingi ya maadili ya kimapokeo ya Kiafrika na linashughulikia masuala ya kijinsia na mengine yanayohusiana nayo katika mazingira ya kijamii na kiitikadi ya Kiafrika.

Mwasisi wa nadharia hii, Steady (1981) anatambua kuwa dhuluma ambazo zimekuwa zikimkandamiza mwanamke wa Kiafrika ni kama vile; kutoweza kuchagua kuwa mzazi au mke wa mtu, ukeketaji wa wanawake, kulazimishwa kunyamaza, unyanyasaji wa kigeni unaotoka nje, urithi

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

wa mali na hata maonevu kwa wanawake tasa. Kutokana na haya Steady (1981) anadai kuwa ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika unafaa kuchunguza hali za kijamii na kitamaduni zinazochangia katika unyanyasaji wa wanawake wa Kiafrika. Anaeleza kwamba ufeministi wa Kiafrika unajumuisha ubaguzi wa rangi, jinsia na wa kitamaduni ili kuibua aina ya ufeministi ambayo ni jumuishi zaidi na ambayo kwayo wanawake hutazamwa kwanza kabisa kama binadamu wala si viumbe ashiki. Juhudi zake zinachochewa na haja ya kumkomboa mwanamke mwafrika kutokana na ubaguzi wa kitamaduni na kidini.

Njogu na Chimera (1999) wanafafanua mihimili ya kimsingi ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ifuatavyo; Moja, ufeministi wa Kiafrika ni jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali anamojipata mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo. Pili, mtazamo wa ufeministi wa Kiafrika hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa `kike wanaoweza kuigwa na ambao hawategemei wanaume ili kujitambulisha na ambao kisaikolojia ni wanawake wanaojitambua na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wenye udhaifu kwa ajili ya umenke wao.

Nadharia hii inanuia kuleta usawa wa wanadamu kwa upande wa jinsia na utamaduni. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za binadamu na wala si za kimaumbile na za kijadi. Ni mtazamo unaokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa. Lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kutokana na utamaduni unaompendelea mwanamume huku ukimdunisha mwanamke. Pia inanuia kuchunguza historia ya fasihi ya jadi ya kike na kuwamulika waandishi wa kike waliotambua hali za wanawake na ambao wanaweza kuchukuliwa kama vielelezo kwa wasomaji wao.

Maelezo ya Wamitila (2003) na Wafula na Njogu (2007) yanaafikiana na maelezo ya Christian (1985) na Miller (1990) kuwa ufeministi wa Kiafrika ni tapo linalopigania haki za wanawake katika muktadha wake wa Kiafrika kwa kumuweka mwanamke mwafrika kati na kuzingatia kwamba anakumbwa na matatizo mengi yanayotokana na utamaduni wake wa Kiafrika. Christian (1985) anahoji kwamba kipengele muhimu kinachotambulisha ufeministi ni ule uwasilishaji ung'amuzi wa kibinafsi wa mwanamke wa Kiafrika ambaye anachukua hatua kuu ya kujikomboa. Miller (1990) akitofautisha ufeministi wa Kiafrika na wa kimagharibi anasema kwamba ufeministi wa Kiafrika huchunguza masuala ya kijinsia kwa mtazamo wa Kiafrika na kuchanganua nafasi ya mwanamke wa Kiafrika katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni na kutathmini jinsi maeneo haya yanamdhalilisha mwanamke.

Kwa mujibu wa Bressler (2003), ufeministi katika muktadha wa Kiafrika hukabiliwa na utetezi wa haki na nafasi ya mwanamke ukinuia kukomboa mwanamke kutokana na asasi dhalilifu za kitamaduni zinazodhibitiwa na itikadi za kiume na kumpa mwanamke nafasi ya kuchangia katika jamii. Hata hivyo Maduka (2005) anadai kuwa ufeministi wa Kiafrika haupingani na wanaume bali huwapa nafasi na hutilia maanani familia kama asasi ya jamii na wakati ule ule kumtetea mwanamke na nafasi yake pamoja na kukashifu itikadi zozote zinazomkandamiza mwanamke. Katika kuafikiana na maoni tuliyozungumzia hapo awali ni muhimu kutambua sifa tatu ambazo Davies (1987) ametilia mkazo akirejelea ufeministi wa Kiafrika. Sifa hizi tatu zinaendana na utafiti wetu na hivyo tulizitumia katika kufikia malengo yetu.

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Mosi, Davies (1987) anadai kuwa ufeministi wa Kiafrika hujikita katika kuleta mwamko wa wanawake na wanaume kuhusiana na unyanyasaji na mizizi yake. Pili, anasema kuwa ufeministi wa Kiafrika huchanganua elementi chanya za jamii za Kiafrika kama ndoa za mitaala na jamaa hasa kuhusiana na uwajibikaji katika ulezi na ugawaji wa majukumu ya unyumba. Tatu, anadai kuwa ufeministi wa Kiafrika huchambua jamii za Kiafrika ili kupata asasi ambazo ni za maana kwa wanawake na kutupilia mbali zile ambazo zinamdunisha.

Anahitimisha kwa kusema kuwa ufeministi wa Kiafrika huenzi hali ya mwanamke wa Kiafrika kujitegemea, kupenda ushirika, na kwamba kwa mwanamke mwafrika si kawaida kuajiriwa lakini huafiki kwamba kazi inayoleta riziki ni jambo lenye udhabiti. Mawazo haya ya Davies (1987) yana uhusiano mkubwa na utafiti wetu na hivyo tutayazingatia katika kuchambua itikadi na uwezo, na kuhakiki mitagusano inayotokea kati ya mwanamke na mwanamume, nafasi ya mwanamke katika jamii pamoja na majukumu anayopewa.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU)

Utafiti huu umeongozwa na mawazo kutoka nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi. Nadharia hii ilibuniwa miaka ya themanini baada ya utambuzi wa majukumu ya lugha katika kuratibu uwezo na mamlaka miongoni mwa wanajamii. Kabla ya miaka ya themanini, tafiti nyingi zilijihusisha na suala la umilisi wa lugha. Katika kipindi hiki uhusiano baina ya lugha na muktadha uliangazwa chini ya utanzu wa isimu amali. Waasisi wa nadharia hii ni pamoja na Ruth Wodak, Norman Fairclough, Teun Van Djik na Gunther Kress. Kwa mujibu wa Weiss na Wodak (2007) UHU ni mkabala wa kisiasa katika utafiti wa lugha na usemi.

Hufasiriwa kama utathmini wa jinsi jamii-lugha hutumia lugha. Hutambulisha dhana za kiisimu zinazobainisha tanzu tofauti na pia vipengele vya kijamii na kitamaduni vinavyosaidia katika ufasiri na uelewa wa matini mbali mbali na aina tofauti za mazungumzo. Msingi muhimu wa UHU ni ukweli kwamba lugha ni zao la jamii na vile vile huzalisha imani na thamani za jamii ambamo lugha hutumika. Wasomaji au wasikilizaji husalia kuwa wapokezi hai. Rasilimali kuu ya uchanganuzi katika UHU ni matini. UHU huchunguza na kuchanganua matini kutambulisha vyanzo vya kimazungumzo vya mamlaka, utabaka, utawala na upendelevu wa jinsi vyanzo hivi huanzishwa, kudumishwa, kuzuliwa upya na kuumbuliwa katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kihistoria (Van-Djik, na Teun, 1993).

Uchanganuzi hakiki wa usemi ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake hivi kwamba uchanganuzi huu hauwezi kuwekewa mipaka ya kiisimu. Kutokana na kijielezi hiki lugha sharti ichunguzwe kwa misingi ya matumizi yake katika miktadha mbalimbali kutegemea watumiaji wake (Yule, 1993).

Misingi ya nadharia hii inapatikana katika sanaa ya unenaji, isimu jamii, isimu matini na isimu matumizi (Buliba, Gwachi, na Matinde, 2014). Dhana za itikadi, uwezo mgawanyo msonge wa majukumu na uana huchukuliwa kama vibadiliki vya msingi katika ufasiri na ufafanuzi wa matini au usemi. Fowler anaonyesha jinsi ambavyo utaratibu wa usemi unavyoweza kuakisi, kuendesha au kuhalalisha ngazi za mamlaka katika jamii. Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi hutambua uamilifu wa lugha katika jamii (Wodak, 1997) na umuhimu wa lugha hukitwa katika miktadha ya matumizi (Wodak, na Dijik, 2000). Kwa mujibu wa Kress (1985), nadharia hii ni ya kipekee katika uchanganuzi wa lugha. Maksio mahsusi ambayo yametokea kuwa msingi wa nadharia hii ni lugha kama suala la kijamii, kuwa na uhusiano baina ya

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

lugha ya kisayansi na lugha ya kijamii, matini na usemi kuwa viambajengo mwafaka vya lugha katika mawasiliano,makundi ya jamii, taasisi za jamii na kila mwanajamii huwa na maana halisi na thamani ambazo hubainishwa kupitia kwa lugha katika utaratibu mahsusi.

Nadharia hii hudhihirisha na kuchanganua uhusiano wa lugha na ruwaza za kiuwezo. Kiambajengo msingi cha uchanganuzi ni matini au usemi kwani ndicho kipashio muhimu cha mawasiliano. Hivyo basi nadharia hii huchanganua muundo ulio wazi na usio wazi wa mahusiano ya kimamlaka, kiubaguzi, kiuwezo na kiutawala ambayo hudhihirishwa na kushamirishwa na lugha. Fairclough (1989) anabainisha mikakati maalum ya uchanganuzi wa lugha mintarafu ya mahusiano na uwezo, itikadi na mabadiliko ya jamii na utamaduni.

Utafiti wake umejikita kwenye vyombo vya habari. Msingi wa nadharia hii ni kuwa lugha yenyewe haina uwezo wala mamlaka. Bali hupata uwezo huu kutokana na wanajamii wenye kumiliki uwezo katika jamii husika. Hii ndiyo sababu nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi (UHU) huchagua mtazamo wa wale wanaoteswa na kuchanganua kwa kina matumizi ya lugha ya wale wenye uwezo na mamlaka ambao wamewajibika katika kuendeleza hali ya kutokuwa na usawa katika jamii (Buliba na wenzake, 2014).

Matini ni sehemu ya mapambano ya kubainisha tofauti katika itikadi, mamlaka na uwezo unaobainisha mvutano wa kiutawala baina ya jinsia ya kiume na ya kike. Lugha husheheni uwezo katika itikadi, hubainisha uwezo na itikadi hizi na huwa kichocheo cha kudhihirisha na kutathmini mamlaka katika jamii. Nadharia hii hujihusisha na jinsi ambavyo wanajamii hupata na kuendeleza uwezo na mamlaka katika jamii. Pia hubainisha utendakazi wa itikadi katika taasisi za kijamii na vilevile, huonyesha jinsi usemi unavyoundwa na kuongoza mielekeo na matarajio ya wanajamii. Uchanganuzi hakiki wa usemi hutambua umuhimu wa matumizi ya lugha katika miktadha ya jamii na kubainisha utendakazi wa itikadi zinazowakilishwa kupitia kwa lugha. Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi huzingatia matatizo mbalimbali ya kijamii. Hivyo basi ilituwezesha kuchanganua mtazamo wa wale ambao hutwezwa na kuchanganua vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika kuhalalisha ngazi za kiutawala, na kulinganisha na wale wanaohodhi uwezo, njia na nafasi ya kusuluhisha matatizo haya na kudumisha usawa katika jamii.

Nadharia hii imekitwa katika mihimili mitano kwa mujibu wa (Fairclough, 1992). Katika mhimili wa kwanza Nadharia ya (UHU) huchukulia kuwa usemi huwa na maana katika wakati maalum wa historia na katika muktadha mahsusi. Fairclough (1992) anadai kuwa usemi huundwa na jamii. Kwamba matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii inayotumia lugha hiyo. Matumizi ya lugha huathiri jamii na vile vile huundwa nayo. Utafiti huu umechunguza matumizi ya lugha katika nyimbo teule za taarab hivyo kupata mwelekeo kutokana na mhimili huu.

Pili, mfumo wa kiuwezo huhalalishwa na itikadi za kundi mahsusi katika jamii lenye kuhodhi uwezo na mamlaka. Fairclough anasema kwamba kuundwa kwa usemi ni suala kuu katika ushindani wa uwezo na mamlaka. Kaida za usemi huathiriwa na jamii kwa njai fulani ambapo udhibiti wa michakato ya uzalishaji huwa njia ya wazi ya utawala. Kwa jinsi hii vikundi vyenye uwezo hutawala jamii pamoja na asasi zake zote. Katika utafiti huu tuliweza kutathmini uwezo walionao wanaume dhidi ya wanawake ili kubaini kama suala la unyanyasaji limedhihirika kutokana na mamlaka waliyonayo wanaume hao.

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Tatu, Fairclough (1992) anasema kuwa usemi husaidia katika kuunda na kubadilisha maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii. Mhimili huu ulituwezesha kuchanganua vile mahusiano ya kijamii yanavyojitokeza katika usemi wa wanaume na kudhihirisha udhalilishaji wa wanawake.

Nne, usemi huundwa na mahusiano ya kiuwezo na umesheheni itikadi. Utafiti huu umechunguza namna uwezo unavyojitokeza katika semi zinazotumika katika nyimbo teule za taarab na ambazo zinamdhalilisha mwanamke.

Tano, Nadharia ya UHU hudhihirisha jinsi jamii na usemi hujengana. Van Dijk (1997) anaunga mkono hoja hii kwa kutoa madai kwamba nadharia hii huchanganua kwa undani miundo, mikakati na majukumu ya matini na mazungumzo pamoja na mpangilio wa vitendo vya kimawasiliano, kimtindo na kiishara katika harakati za kujenga mahusiano kati ya usemi, imani na jamii ambayo anayachukulia kama pembe tatu za nadharia hii.

Hivyo basi mtazamo wa Wodak wa uchanganuzi kihistoria hutumiwa kwani ni mtazamo ambao hushirikisha maarifa mapana kuhusu asili na usuli wa hali mbalimbali za jamii katika misingi ya kidaikroniki. Mtazamo wa uchanganuzi kihistoria huchukulia lugha kama tendo la kijamii ambapo Wodak (1996) anasisitiza umuhimu wa muktadha wa matumizi ya lugha. Usemi huongozwa na tofauti za kimamlaka ambazo ni sehemu ya jamii. Kwa kutumia mtazamo huu wa kihistoria miundo ya mahusiano ya wanajamii wenye mamlaka, waliotengwa na wenye kumiliki nyenzo za uzalishaji mali huhakikiwa na kuonyesha jinsi miundo hii inavyosimbwa na kudumisha ruwaza za kiuwezo.

Mtazamo huu huwa mwongozo thabiti wa kuwezesha uchanganuzi wa mpangilio wa kijamii. Pia hutumika kudhihirisha namna jamii inavyokuwa imeratibu ngazi za mamlaka na majukumu kiuana kupitia kwa lugha katika nyanja mbalimbali za matumizi ya lugha katika miktadha anuwai ya jamii. Nadharia huwezesha kutambua endapo lugha inayotumiwa katika jamii hujenga, husawiri au kudumisha ruwaza za mahusiano ya kiuwezo katika jamii hiyo. Humwezesha mhakiki kubainisha itikadi zinazotawala mahusiano ya kijamii kwa misingi ya kijinsia na ruwaza za mahusiano ya kiuwezo (Kress, 1985; Buliba na wenzake, 2014). Nadharia hii ilituwezesha kuchanganua nyimbo ambazo zimejikita kwayo katika misingi inayolenga kumnyanyasa mwanamke ili tupate kuelewa mpangilio wa jamii kijinsia.

Fairclough (1989) anapendekeza njia tatu za kufanya uchanganuzi hakiki wa usemi: Moja, uchanganuzi wa matini. Pili, uchanganuzi wa tendo la usemi na maingiliano. Tatu, uchanganuzi wa tendo la jamii (muktadha). Fairclough (1989) anafafanua hatua tatu za kufanya Uchanganuzi hakiki wa usemi ifuatavyo; Hatua ya kwanza ni kufanya ufafanuzi wa sifa rasmi za matini kama vile msamiati, sarufi na miundo ya matini. Pili, Kufanya ufasili unaojihusisha na mahusiano kati ya matini na maingiliano yani tendo la usemi. Kwenye hatua hii matini huangaziwa kama zao la mchakato wa ufasili. Nazo kaida zinazotumiwa hubainishwa na jinsi kaida hizo zilivyotumika huchunguzwa. Tatu, Kupambanua uhusiano kati ya maingiliano (tendo la usemi) na tendo la jamii yani muktadha wa jamii. Hatua hii huchunguza mchango wa usemi kwa tendo la jamii, athari za usemi kwa kuunda maarifa, mahusiano na utambulisho wa kijamii. Hivyo basi, uwezo ndani ya usemi hutokana na washiriki wenye uwezo wa kudhibiti mchango wa wale washiriki wasio na uwezo. Katika nadharia ya UHU msisitizo huwekwa upande wa uteuzi wa neno na matumizi yake katika usemi. Umuhimu wa nadharia hii katika utafiti huu ni kutumika katika uchanganuzi wa matini za nyimbo teule za taarab na kubaini jinsi masuala

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ya unyanyasaji yanavyojitokeza kutokana na wenye uwezo kuwadunisha wasio na nguvu katika jamii.

Suala la jinsia na majukumu

Halliday amechunguza dhamira na uteuzi wa msamiati ili kudhihirisha usawa uliopo kijinsia na kueleza kuwa lugha katika riwaya imetumika kumdunisha mwanamke hivi kwamba mwanamume amepewa nafasi ya juu zaidi katika kutekeleza majukumu mbali mbali huku mwanamke akisalia na uwezo mdogo wa kujikomboa au hata bila namna yoyote ya kumuwezesha kujikwamua (Halliday, 1985). Utafiti huu umetufaa katika uchanganuzi hakiki semi ili tuelewe namna lugha kwa ujumla inavyotumika kumsawiri mwanamke. Katika kuchunguza mahusiano ya kijinsia katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (Matei, 2014) amebaini kwamba mahusiano ya kijinsia yapo na yamemsawiri mwanamke kama kiumbe aliye mnyonge.

Ametumia riwaya katika utafiti wake nasi tumetumia matini za nyimbo za taarab. Utafiti wake umetufaa katika kuelewa namna mwanamke anavyosawiriwa na wasanii mbali mbali katika riwaya. Kwamba, si waimbaji tu wanaomchora mwanamke kuwa duni bali pia wasanii katika Fasihi andishi huwachora wanawake kihasi. Katika riwaya ya *Kasri Ya Mwinyi Fuad*, anavyohakiki (Senkoro, 2011) mwanamke amesawiriwa akiwa mnyonge, vile vile katika riwaya za *Kiu na Nyota ya Rehema*. Pia *Utenzi wa Mwana Kupona* ni kielelezo cha unyonge wa mwanamke katika mfumo wa kimwinyi ambako malezi ya wazazi wake, hata ya mamake mwenyewe, yanamfunda amnyenyekee, amtumikie na kumtii pamoja na kumwogopa mumewe ambaye tunaelezwa kupitia kwenye utenzi huu, haifai ajibiwe hata kama amefanya makosa kwani yote yataamuliwa na Mungu (Mulokozi, 1999).

Usawiri wa Mwanamume katika Wimbo wa *V.I.P*

Mwanamume amejisawiri kama mtu maalum anayependwa sana na mwanamke. Amejipa uwezo na nguvu nyingi ambapo anasema wale watu wengine ni ovyo. Mwanamume anajiita *Very Important Person* akimaanisha '*mtu wa maana*.' Anapewa huduma zote anazohitaji zikiwemo za kimapenzi na kutimiziwa haja zake jumla. Kwa hivyo mwanamke anasalia kuishi katika kivuli cha mwanamume kwa kumtumikia.

Katika ubeti wa kwanza anasema:

…Mimi VIP, wao wawe ovyo
…Mimi VIP, wao wawe ovyo….

Mwanamume anaona kwamba yeye akiwa *mtu wa maana* basi watu wengine hawana umuhimu, ila anadai katika mstari ufuatao kwamba anapohitaji huduma ya mwanamke sharti ahudumiwe tena atimiziwe mambo fulani.

Mwanamke kama mhudumu wa mwanamume

Mwanamume anajipatia uwezo wa kiitikadi wa kuona kwamba yeye ndiye bora zaidi huku mwanamke akisalia kuwa duni. Japo anamdunisha mwanamke anatambua uwezo wa kutumikiwa na mwanamke yuyo huyo upo katika kutimiziwa mahitaji yake anaposema:

Panapo huduma akuhudumie, na mambo fulani akutimizie

Mwanamume anaposema mambo fulani akutimizie alimaanisha kutimiziwa haja zake za kimapenzi. Anaposema 'wao wawe ovyo' anamaanisha kwamba watu wengine hususan wanawake hawana uwezo kama yeye na hiyo inaonyesha anavyodunisha wanawake. Mwanamume anapojiita *V.I.P* akimaanisha kuwa yeye ni *very important person* yaani mtu wa maana anajiona kuwa mwenye thamani kuliko mwanamke na ndio chanzo cha kutaka afanyiwe kila jambo analotaka. Hii inatokana na mfumo hasi wa jamii inayomweka mwanamume juu huku mwanamke akiwekwa chini

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kutokana na utamaduni pamoja na itikadi zake. Katika ubeti wa pili mwanamume anasema:

Wanaume tumepewa daraja kubwa na Mungu
Mashababi tumekuwa na kila aina ya mizungu
Kila unapozidiwa, huna ujanja mwanangu
Mimi ninavyoenziwa, first class walimwengu
Vile ninahudumiwa, nimepanda daraja yangu
Penye sifa husifiwa, VIP nafasi yangu

Mwanamume anadai kwamba amepewa daraja akiwa na maana ya kwamba amepewa uwezo mkubwa na Mungu wa kumtawala mwanamke. Anafurahia anavyopendwa na kupewa heshima ndio maana anasema anapewa huduma ya *first class* ambayo ni bora zaidi. Pia anadai kusifiwa na kutengewa nafasi maalum katika jamii.

Usawiri wa Mwanamke kama Chombo cha Starehe

Wimbo huu wa *V.I.P* unampa mwanamume uwezo wa kumtawala mwanamke na kujiona bora zaidi. Jambo hili linatuelekeza katika kuelewa mahusiano ya uwezo kati ya manamke na mwanamume katika jamii. Matokeo ya itikadi na uwezo wa kijinsia yakiwa kwamba mwanamke anaonekana kunyanyaswa kwa kumfanyia mwanamume mambo mengi. Wimbo huu wa *V.I.P* unaonyesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanamume. Japo ni utamaduni wa jamii, mambo kama hayo yanamweka mwanamume juu na mwanamke chini katika mahusiano ya mamlaka na ukosefu wa usawa huo unaotokana na itikadi ya ubabedume. Mwanamke amesawiriwa kama asiye na nguvu wala mamlaka yoyote katika jamii. Amechorwa kama mhudumu wa mwanamume kulingana na utamaduni wa jamii. Kazi yake ni kumtumikia na kumsifu mwanamume. Hali hii inamtia mwanamke katika utumwa wa hali fulani maana anakuwa mtu wa kumfurahisha tu mwanamume kupitia kwa matendo yake. Usawiri wa mwanamke umejitokeza kiitikadi kama anayetegemea matendo ya mwanamume na hivyo nafasi yake katika mahusiano yake na mwanamume inakuwa iliyopembezwa. Suala hili japo ni la utamaduni inaishia kuonekana kama utumwa wa aina yake. Utumwa huu ni njia ya kudumisha itikadi kama vile ya kibabedume. Mwanamke ndiye wa kumpepea mume anapokula na kumsugua mwili inapobidi kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao:

Mimi nikipewa raha, wengine wanachukia
Acheni nipewe raha, zote raha za dunia
Nikila na pepewa, na mwili na suguliwa

Kudunishwa kwa mwanamke katika wimbo wa *Daktari wa Mapenzi*

Katika wimbo wa *Daktari wa Mapenzi* mwanamume anajiona kuwa daktari wa mapenzi, kwamba yeye ndiye tiba ya mwanamke. Anajivuna kwamba amejaliwa taaluma ya kuyatibu mapenzi. Hivyo mwanamume anajipatia uwezo wa kushughulikia matatizo yote yanayomkumba mwanamke huku akijiita bingwa wa kutibu mapenzi. Katika ubeti wa kwanza anasema;

Yote yalotokezea, yote yalotokezea ni baraka za Muumba
Kanitunukia kanitunukia namshukuru Muumba
Taaluma nimejaliwa, ya kuyatibu mapenzi
Mgonjwa akizidiwa, namtibu bila ganzi
Nawatibu wenye wivu, ulozidi kwenye penzi
Nayotoa makovu, yalozidi kwenye penzi
Mi ndo daktari bingwa, wa kuyatibu mapenzi

Mwanamume anatumia neno taaluma akiwa na maana kuwa anajua jinsi ya kufanya mapenzi na ndio uhodari alio nao. Ndio maana anajinaki na kujipatia lakabu ya 'daktari wa mapenzi.' Anaposema kwamba anatibu bila ganzi anamaanisha kwamba hashindwi katika ile kazi anayoizungumzia. Katika ubeti ufuatao anasema kwamba yeye ni daktari wa mapenzi kimiujiza. akitumia

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

lugha ya Kiingereza kuonyesha kuwa ni msomi. Hata hivyo anamaanisha yeye si daktari wa kweli anaposema:

> *Helua helua by miracle ni daktari wa mapenzi*
> *Mashaallah, Mashallah, ni tabibu hodari wa kuyatibu mapenzi,*
> *Nyenzo zangu luxury ni specialist wa enzi…*
> *Mwenye presha ya mapenzi, anayependa hajiwezi*
> *Kuwashwa washwa kwa mapenzi, mi ndo wake muuguzi.*

Kwa kutumia maneno kama vile luxury (anasa) ni specialist (mtaalam) anadhamiria kueleweka kwamba yeye anapenda anasa na ni mtaalam wa kila ugonjwa ikiwemo *presha*.

> *Najulia kupasua, bila kutoa vidonda*
> *Najua kumtibia, mwenye wivu wa kukonda*
> *Mwenye presha, presha inatulia, mwenye shegesha maradhi yanatulia*
>
> *Sina presha kwenye taaluma yangu, nakula maisha silali njaa wenzangu*
> *Sina presha kwenye taaluma yangu, nakula maisha silali njaa wenzangu*
> *Nina kitengo cha massage cha kuchua na kukanda, namtibu mjuaji, mnene na alokonda*
> *Siogopi chochote nasema sijali chochote, sijali chochote,*
> *Nafanya makusudi, eeh nafanya kusudi acha weee*
> *Nafanya makusudi, eeh nafanya kusudi acha weee*

Kwa ujumla katika wimbo huu mwanamume anaonyesha ubabedume kwamba anaweza kila kitu hususan kinachoendana na masuala ya mapenzi na ndio maana anajiita *daktari wa mapenzi*. Anajiona kuwa hodari katika masuala ya unyumba ila hamthamini mwanamke ambaye ndiye mwanandoa- mwenza anapodai kwamba kila anachokifanya kina kusudi. Anaporejelea kwamba anawatibu mjuaji, mnene na alokonda anadhihirisha ubabedume. Istilahi kama hizo pia zinadhihirisha kumdunisha mwanamke kwamba ni mjuaji, alokonda. Fauka ya hayo ni wazi kwamba mwanamume anapewa nafasi ya kushiriki mapemzi na wanawake tofauti tofauti katika jamii ishara ya uwezo kiume.

Hitimisho

Makala hii imebaini kuwa japo wanawake wanatekeleza majukumu muhimu katika jamii wanasawiriwa kwa mtazamo hasi. Katika nyimbo mbili tulizochanganua mwanamke anamtunza mwanamume katika hali zote lakini bado anadunishwa kwa kuonekana ovyo. Mwanamume anajipatia uwezo mkubwa wa kumtawala mwanamke huku akijiita daktari tena mtu maalum. Ina maana kwamba mwanamke ndiye mgonjwa anayestahili tiba kutoka kwa mumewe. Lugha imetumiwa kama chombo cha kudhihirisha mahusiano ya mamlaka katika jamii. Hii ina maana kwamba lugha imefanywa kukuza na kuendeleza matakwa ya wenye nguvu kwa kufanya mawazo hayo yaonekane. Utafiti umegundua kwamba mwanamume anapotunga wimbo na kuwafanya wanawake waimbaji katika nyimbo hizo, anataka kuendeleza na kudumisha ubabedume. Anahakikisha kwamba mahusiano ya kiitikadi kati yake na wanawake yanasalia katika kiwango cha mwanamke kukosa uwezo wa kujikimu na hivyo kuwa mtegemezi wa mwanamume. Kwa hivyo ni wazi kuwa itikadi ya ubabedume wanayotaka kukuza imetawala katika nyimbo hizi.

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

MAREJELEO

Beauvoir, S. (1952). *The second sex.* New York: Modern Library.
Bressler, C. E. (2003). An Introduction to Theory and Practice Literary Criticism.
Buliba, A., Gwachi, M., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
Christian, B. (1985). Black feminist criticism perspectives on black women writers.
Davies, C.B. & Graves A., (1987) Ngambika: Studies of Women in African Literature. *The International Journal of African Historical Studies* vol, 20 no1
Fairclough, N. (1992). *Language and Awareness.* London: Longman Publishers.
Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse analysis: The critical study of language.* London: Longman Publishers.
Fairclough, N. (1989). *Language and power.* London: Longman Publishers.
Greer, G. (1971). *The female eunuch.* New York: McGraw.
Halliday, M. A. (1985). 1994. *An introduction to functional grammar*, 2.
Igobwa, S. (2007). Taarab and chakacha in East Africa: Transformation, appreciation and adaptation of two popular music genres of the Kenyan coast. *A Paper Presented during a Conference on Music in the World of Islam*, (pp. 8-13). Toronto, Canada.
Kinge'i, K. G. (1992). *Language culture and communication: The role of Swahili taarab songs in Kenya.* Washington, DC: Ann Arbor University Microfilms.
Kobia, J. M. na Mung'ahu, R. (2011). 'Ubabedume katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Utenzi wa Fumo Liyongo' katika *Kioo cha Lugha* Juzuu 11, Dar es Salaam: Dar es Salaam University.
Kress, G. (1985). *Linguistic processes in sociocultural practice*. Victoria: Deakin University.
Leslie, O. (1990). Molara.". *Interview." In Their Own Voices: African Women Talk. Ed. Adeola James. London: James Currey*, 65-73.
Matei, A. (2014). *Discourse, Gender and Gender power relations in fiction.* Nairobi: Unpublished Thesis.
Maduka C.T (2005) *African and Comperative Literature in Era of Globalization* in Chidi T. and Denis E.EDS. Compass essays in Honourof Wilfred F. Feuser. PortHarcout.
Miller, F. (1990). *Latin American feminism and the transnational arena*. na.
Momanyi, C. (2001). *Nadharia ya Uchunguzi Nafsia katika mtazamo wa kike na uhakiki wa kifasihi katika kioo cha lugha.* Dar es Saalam: Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.
Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Saalam.
Njogu, K. & Chimera, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.
Ntarangwi, N. (1998). *Music, Gender and Islam in East Africa urban context.* Illinois: University Microfilms.
Senkoro, F. (2011). *Fasihi.* Dar es Salam: Kauttu Limited.
Showalter, E. (1977). *A literature of their own: British women novelists from Brontë to Lessing* (p. 14). Princeton: Princeton University Press.

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | May-2020|
Received: 02.05.2020; Accepted 08.05.2020; Published: 30.05.2020 at www.editoncpublishing.org
Malenya Mary et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Steady, C.F. (1981). *The black woman cross-culturally.* Schenkman.
Van, D., & Teun, A. (1993). *Critical Discourse Analysis; Discourse and Society* (Vol. 2). (4th Ed.)
Van Dijk, T. A. (1997). Opinions and ideologies in the press.
Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi,istilahi na nadharia.* Nairobi: Focus Publisher.
Weiss, G., & Wodak, R. (Eds.). (2007). *Critical discourse analysis*. New York, NY: Palgrave Macmillan.
Wodak, R. (1996). *Critical Linguistics and critical analysis: Handbook of pragmatics.* Amsterdam: Benjamins.
Wodak, R. (1997). *Gender and Discourse.* London: Sage publishers.
Wodak, R., & Dijik, T. A. (2000). *Racism at the top. Parliamentary discourses on ethnic issues in six European states.* Klagenfurt: Drava.
Wodak, R., & Meyer, M. (2001). *Methods of Critical analysis: Introducing qualitative methods.* London; New Delhi: Oaks and Sage Publications.
Wollstonecraft, M. (1792). *A vindication of the rights of woman.* Boston: Peter Edes.
Woolf, V. (1929). *A room of one's own.* London: Hogarth Press.
Yego, E.K. (2011). *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab Zanzibar*: Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
Yule, B. (1993). *Discourse analysis.* New York: Cambridge University Press.

© 2019, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org